**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA UCHUMI NA UWEKEZAJI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

*[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 124 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Toleo la Februari, 2024]*

**May, 2026**

## 1.0 SEHEMU YA KWANZA

## 1.1 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,**

Sina budi kumshukuru Allah (S.W.T) mwingi wa rehma na utukufu, kwa kutujaalia uhai na Afya njema, na kutuwezesha kuendelea kutekeleza jukumu la Kikatiba kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Aidha nikushukuru na kukupongeza wewe **Mheshimiwa Spika,** kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi na upeo mkubwa. Ni imani yangu kwamba, utaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu cha kuwatumikia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia,naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la mapinduzi Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuendelea kuiletea Zanzibar maendeleo makubwa na haraka kwa wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, nampongeza Mhe. Waziri, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Mhe. Masoud Ali Mohammed, Naibu Waziri Mhe. Mboja Ramadham Mshenga , Katibu Mkuu,Kaptain Hamad Bakar Hamad, Naibu Katibu Mkuu Zahour Kassim Mohammed pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada kubwa wanazozichukua katika kusimamia jukumu la Wizara ya Uchumi Buluu na Uvuvi Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Uchumi na Uwekezaji kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati, Wajumbe wa Kamati wameweza kuijadili ipasavyo Bajeti ya wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha fedha wanazoidhinisha katika Baraza hili, zinatumika vizuri kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, na kwa heshima ya kipekee naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| i. | Mhe. Makame Mohammed Sufiani | Mwenyekiti |
| ii. | Mhe Dr. Mahmoud Omar Mohammed | M/Mwenyekiti |
| iii. | Mhe. Alley Masoud Alley | Mjumbe |
| iv. | Mhe. Shafi Mohammed Shafi | Mjumbe |
| v. | Mhe. Chumu Kombo Khamis | Mjumbe |
| vi. | Mhe. Tabia Maulid Mwita | Mjumbe |
| vii. | Mhe. Toufiq Salim Turky | Mjumbe |
| viii. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| ix. | Ndg. Abdu Maulid Haji | Katibu |
| x. | Ndg. Shaaban Suleiman Juma | Afisa Bajeti |

**Mheshimiwa Spika, kwa** mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Toleo la Februari, 2024, nawasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Uchumi na Uwekezaji ya Baraza la Wawakilishi, Zanzibar

Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi matakwa ya Kanuni ya 124(2) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

i. Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya Utangulizi pamoja na kuelezea msingi iliyotumika katika uandaaji wa Taarifa hii pamoja na namna Kamati Uchumi na Uwekezaji ilivyofanya kazi;
ii. Sehemu ya Pili imebeba taarifa ya uchambuzi juu ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
iii. Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii inaonyesha uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027;
iv. Sehemu ya Nne imebeba Maoni pamoja na Ushauri wa Kamati baada ya uchambuzi uliofanyika; na
v. Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuaji wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa uchambuaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi unatokana na matakwa ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, 2024. Kanuni ya 119(3) zinaipa Kamati hii miongoni na majukumu mengine, jukumu la kufanya uchambuzi wa Bajeti na Makadirio ya Wizara hii.

Aidha, Kanuni ya 101 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Zanzibar Toleo la mwaka 2024 imeweka masharti yanayoelekeza kuwa Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati ya Uchumi na Uwekezaji kabla ya kujadiliwa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar.

Hivyo, naomba kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa masharti hayo yaliyoelekezwa katika Kanuni zetu za Baraza yamezingatiwa na kwamba naliomba Baraza lako Tukufu liijadili hoja ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na Taarifa hii ya Kamati ya Uchumi na Uwekezaji.

### 1.3 Maeneo ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara Uchumi wa Buluu inagusa **Fungu moja Nambari 013** lenye Programu Kuu tatu (3) na ndogo 7 ambazo ni:

I. Programu Kuu ya Maendelero ya Uchumi wa Buluu **(P01)**

II. Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi **(P02)**

III. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi **(P03)**

Naomba kutoa taarifa mbele ya Baraza lako Tukufu kuwa, Kamati ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Programu zote tatu Pamoja na Programu ndogo zilizoambatana na Programu Kuu.

## 2.0 TAARIFA YA UCHAMBUZI NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi unaweka msingi ya Kikanuni kwa Kamati hii kutoa ushauri unaohusiana na Hoja hii ya Wizara ya Uchumi wa buluu na Uvuvi ambapo uchambuzi wetu ulijielekeza katika maeneo makuu yafuatayo; -

i. Makusanyo ya mapato;
ii. Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia 2025/2026;
iii. Muelekeo wa Wizara katika Bajeti ya 2026/2027
iv. Uchambuzi wa matumizi na Makusanyo ya Mapato
v. Utekelezaji wa maagizo ya Kamati.

### 2.2 MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilikadiriwa kukusanya **Shilingi 11,273,214,000** kutoka vyanzo vyake vya makusanyo na hadi kufikia Machi 2026, Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 8,493,203,472** kati ya **Shilingi 9,261,573,363** zilizokadiriwa sawa na **asilimia 92** kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi, 2025/2026). Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 75** ya makadirio ya mwaka.

**MATUMIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ililiomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha **Shilingi 172,033,961,377** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, Wizara imeingiziwa jumla ya **Shilingi 35,116,155,652** sawa na **asilimia 20.4 tu** ya makadirio ya mwaka.

**Mheshimiwa Spika,**tathmini ya Kamati kuhusu upatikanaji huo wa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeona kuwa ulikua si wa kuridhisha katika utekelezaji wa shughuli za Wizara, Hivyo kamati inaishauri Serikali kuangalia athari zitokanazo na hali hiyo ili kuona bajeti ya matumizi ya mwaka mpya wa fedha 2026/2027 inakua ya mafanikio.

## 3.0 MAPITIO YA MATUMIZI NA MAPATO KWA FUNGU LA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI (013) KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**MATUMIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka huu wa fedha 2026/2027 wizara imeliomba Baraza lako Tukufu kuidhinishiwa matumizi ya **Shilingi 209,007,499,000** kwa **Fungu la Bajeti 013** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuongezeka kwa bajeti ya matumizi kutoka **shilingi 172,033,961,377** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia **shilingi 209,007,499,000** kwa mwaka wa fedha

2026/2027. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kuwa na bajeti zaidi ya matumizi katika mwaka mpya wa fedha ili kuweza kukabiliana ipasavyo na utekelezaji wa shughuli mbali mbali za Uchumi wa Buluu na Uvuvi zilizopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa miongoni mwa changamoto za msingi za Wizara ni uhaba wa rasilimali fedha katika uendeshaji wa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC). Hivyo Kamati inaishauri serikali kuizingatia zaidi bajeti ya matumizi ya  Kampuni hiyo ili kuweza kufikia malengo ya serikali ya upatikanaji wa rasilimali ya mafuta na gesi asilia  nchini.

## MAKADIRIO YA MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imekadiriwa kukusanya **Shilingi 13,251,303,000** ikiwa ni mapato yatakayokusanywa kupitia vyanzo vya Makusanyo,

**Mheshimiwa Spika,** makadiro ya mapato katika mwaka huu wa fedha yameonekana kuongezeka kutoka  **Shilingi 11,273,214,000** kwa mwaka 2025/2026 hadi kufikia **Shilingi 13,251,303,000** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa ongezeko hilo limetokana na sababu zifuatazo:

1. Kuongezeka kwa viwango vya tozo za viingilio  katika sehemu za Hifadhi za Bahari zinazotumika kwa shughuli za utalii.
2. Juhudi za ukusanyaji mapato kupitia mifumo rasmi
3. Kuanzishwa kwa Hifadhi nyengine mbili mpya (Hifadhi ya Kaskazini Mashariki na Kusini Mashariki) Pemba.

Hivyo, Kamati inapongeza juhudi za Wizara kwa kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitakwenda kusaidia katika ukusanyaji wa mapato katika mfuko mkuu wa Serikali.

## 3.1 UTEKELEZAJI WA MAELEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishukuru Wizara ya Uchumi wa Buluu kwa kuendelea kutekeleza maelekezo ya Kamati .Kamati yetu ya Uchumi na Uwekezaji imeridhika ufanyaji kazi wa Wizara katika kutekeleza Sera ya Serikali ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

## 4.0 MAONI YA JUMLA YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia uchambuzi kuhusu Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Kamati hii inatoa maoni ,ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu na Programu zote kama ifuatavyo:

1. Kamati imebaini kuwa bado kuna umuhimu mkubwa kwa Wizara kutoa elimu kuhusu Sera ya Uchumi wa Buluu katika medali ya Makongamano ya Ndani na Nje ya nchi .

2. Kamati inaikumbusha Wizara kuhakikisha kuwa suala la fidia kwa wananchi wenye maeneo ya miradi linasimamiwa ipasavyo ili wananchi wanaostahili kupatiwa fidia waweze kupatiwa,kwani ni haki yao .

3. Kamati inaishauri Serikali/Wizara kuongeza kutoa elimu na taarifa kwa jamii kuhusu suala la upatikanaji wa rasilimali ya Mafuta na Gesi asilia Zanzibar. Kamati imebaini kuwa uelewa wa wananchi hivi sasa kuhusu maendeleo ya Mradi huo upo vyengine kutokana na kutopatikana kwa taarifa zilizohai na endelevu za mradi huo.

4. Kamati inaishauri Serikali/Wizara ili kuhakikisha uwekezaji katika sekta ya mafuta na gesi asilia unafanikiwa Zanzibar, ipo haja ya kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa rasilimali fedha za ufuatiliaji, wataalamu katika kada hiyo na kushiriki ipasavyo katika mikutano mbali mbali ya kidunia yenye lengo la kutangaza uwekezaji huo.

5. Kamati inaishauri Wizara kufanya mabadiliko ya Sheria ya Uvuvi itakayoanzishwa itakayozikabili changamoto zilizopo katika maendeleo ya Uvuvi.

6. Kamati inapongeza mpango wa Serikali wa kununua Meli 2 kwa ajili ya Uvuvi wa Bahari kuu sambamba na Mpango wa kuanzisha Mradi wa ujenzi wa Bandari mpya ya Uvuvi Zanzibar.

7. Kamati inaishauri Serikali/Wizara kuwekeza kwa ajili ya uendeshaji wa utafiti kuhusu mahitaji ya uvuvi. Kamati imebaini kuwa suala la utafiti katika eneo hilo linahitaji bajeti kubwa katika utekelezaji wake.

8. Kamati inaishauri Wizara kuwa na mipango endelevu ya kuandaa miundo mbinu ya kuwafikia Samaki kwani Kamati imebaini kuwa miundo mbinu iliyopo haikidhi haja katika soko la Uchumi wa buluu..

9. Kamati inashauri serikali /wizara kufanya utafiti wa zao la mwani katika maeneo ya Pemba ambapo zao hilo linaonekana kupotea hivi sasa.

10. Kamati imebaini kuwa bado kunahitajika mipango endelevu na ya kimkakati kuhusu Mradi jumuishi wa kuwaendeleza wanawake wanaojihusisha na kilimo cha zao la mwani nchini.

11. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na vyombo vengine kusimamia ipasavyo Sheria ya Uhifadhi wa Bahari katika suala la usafi.

12. Kamati inaishauri wizara kuwa ujenzi wa Chuo cha Uvuvi katika eneo la Shumba Mjini kuuzingatia kwa umuhimu wake kwani umuhimu wa kuwepo kwa Chuo hicho katika eneo hilo ni mkubwa.

13. Kamati inaishauri wizara kufanya mapitio ya utaratibu wa utoaji wa leseni za mabaharia kwani ipo haja ya kuangalia mifumo ya upatikanaji wa Leseni hizo ili kuondoa urasimu uliopo.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha Hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono Bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba Kamati yangu naunga mkono hoja.

Naomba kuwasilisha.

.....................................................

**(Mhe. Makame Mohammed Sufiani)**

Mwenyekiti,

Kamati ya Uchumi na Uwekezaji,

Baraza la Wawakilishi,

**<u>Zanzibar.</u>**